ISSN: 0856 - 8030

The
# Regulator

Linatolewa bure

JARIDA LA KILA ROBO MWAKA LA MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA

ISSN: 0856 - 8030 NA. 3/2023 JULAI - SEPTEMBA 2023




# Tanzania yajiimarisha kama kitovu cha Posta Afrika

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**

**ISO 9001:2015 CERTIFIED**

# TAARIFA KWA UMMA

## UTOAJI WA HUDUMA ZA MAWASILIANO BILA LESENI

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) inapenda kuutaarifu Umma kuwa utoaji wa huduma za mawasiliano, zikiwemo huduma za usalama mtandaoni (cybersecurity services), intaneti, na vituo vya kutunzia data (data centres), katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania bila kuwa na leseni iliyotolewa na TCRA ni kinyume na Kifungu cha 14 cha Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta ya mwaka 2010 (EPOCA) ambacho kinakataza mtu, taasisi au kampuni yoyote kutoa huduma hizo bila kuwa na leseni.

Aidha, tunapenda kuukumbusha Umma kuepuka kutumia huduma za mawasiliano, zikiwemo huduma za usalama mtandaoni, intaneti, na vituo vya kutunzia data, zinazotolewa na mtu, taasisi au kampuni zisizo na leseni zilizotolewa na TCRA.

TCRA inaendelea kusimamia huduma za mawasiliano nchini na haitasita kuchukua hatua kisheria dhidi ya mtu, taasisi au kampuni itakayobainika kujihusisha na utoaji wa huduma za mawasiliano, zikiwemo huduma za usalama mtandaoni, intaneti na vituo vya kutunzia data, ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania bila kuwa na leseni iliyotolewa na TCRA

Kwa taarifa zaidi wasiliana nasi kupitia nambari 0800 008 272 au baruapepe: dawatilahuduma@tcra.go.tz .

Dkt. Jabiri K. Bakari
**MKURUGENZI MKUU**

Jengo la Mawasiliano, Na. 20 Barabara ya Sam Nujoma, S. L. P 474, 14414 DAR ES SALAAM, TANZANIA.
**Simu:** +255 22 2199760-9 / +255 22 2412011-2 / +255 784558270-1 **Nukushi:** +255 22 2412009-10
**Barua pepe:** barua@tcra.go.tz, dg@tcra.go.tz, **Tovuti:** www.tcra.go.tz

ISSN: 0856 - 8030
NAMBA YA USAJILI: 00000115
Na. 3/2023. JULAI - SEPTEMBA, 2023

# The Regulator

Hili ni toleo la Kiswahili la jarida la The Regulator, linalotolewa mara nne kwa mwaka na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA). TCRA ni taasisi ya serikali inayosimamia mawasiliano ya kielektroniki na posta nchini. Jarida hili ni sehemu ya utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka.

## TCRA ina wajibu katika majukumu yafuatayo:-

1. Kuhimiza ushindani bora na uchumi wenye tija;
2. Kulinda haki na maslahi ya watumiaji;
3. Kuhamasisha upatikanaji wa huduma za mawasiliano kwa watumiaji wote (wakiwemo Walemavu) ukijumuisha watumiaji wenye kipato kidogo, walioko vijijini na watumiaji ambao wako katika maeneo yasiyokuwa na mvuto wa kibiashara;
4. Kuimarisha elimu kwa umma, uelewa na kuzifahamu huduma zinazosimamiwa;
5. Kuhakikisha umuhimu wa kulinda na kutunza mazingira.

## BODI YA WAHARIRI

**Mwenyekiti**
Mhandisi Mwesigwa Felician

**Katibu**
Bw. Rolf Kibaja

**Wajumbe**
Bw. Semu Mwakyanjala (Mratibu)
Dkt. Philip Filikunjombe
Dkt. Peter Kihogo
Bw. Peter Lyimo
Bw. Robin Ulikaye
Bw. Abel John
Bi. Vitalia Kidabulo
Bw. Alpha Wawa

**Mhariri Uzalishaji**
Bw. Isaac Mruma

**Anwani ya ofisi za uhariri**

Jengo la Mawasiliano, Na. 20 Barabara ya Sam Nujoma, S.L.P 474,
Postikodi 14414 Dar es Salaam.
Simu: +255 784558270, +255 784558271. Barua pepe: regulator.magazine@tcra.go.tz; dg@tcra.go.tz

@tcra_tanzania

**Ofisi Kuu**
Jengo la Mawasiliano, Na. 20 Barabara ya Sam Nujoma,
S.L.P 474,
Postikodi 14414 Dar es Salaam.
Simu +255 784 558270-1 Simu ya bure: 0800008272.
Barua pepe: dg@tcra.go.tz. Tovuti: www.tcra.go.tz

**Ofisi ya Zanzibar**
Na. 19 Mbuyukisutu, Mjini Magharibi, Zanzibar.
S.L.P 3284,
Postikodi 71194 Mjini Magharibi
Simu: +255 24 2235062
Baruapepe: zanzibar@tcra.go.tz

**Kanda ya Kaskazini**
Jengo la PAPU, Ghorofa ya kumi na mbili. 280 Barabara ya Moshi-Arusha. S.L.P 15675,
Postikodi 23194 Arusha.
Simu: +255 272970286
Baruapepe: arusha@tcra.go.tz

**Kanda ya Kati**
LAPF Plaza, Ghorofa ya nne. Na. 2 Mtaa wa LAPF.
S.L.P 2229,
Postikodi 41194 Dodoma. Simu: +255 262321731
Baruapepe: dodoma@tcra.go.tz

**Kanda ya Nyanda za Juu Kusini**
Jengo la NHIF, Ghorofa ya tano. Na. 7 Barabara ya Karume.
S.L.P 1375,
Postikodi 53194 Mbeya. Simu: +255 25 250 5016
Baruapepe: mbeya@tcra.go.tz

**Kanda ya Ziwa**
Jengo la NSSF Mafao, Ghorofa ya nne, upande B Na.13
Jomo Kenyatta Avenue.
S.L.P 3108,
Postikodi 32194 Mwanza. Simu: +255 28 2505082,
Baruapepe: mwanza@tcra.go.tz

**Kanda ya Mashariki**
Na.147 Barabara ya Kajenge, Mikocheni,
S.L.P 35615,
Postikodi 14194 Dar es salaam.
Simu: +255 22 2775110
Baruapepe: easternzone@tcra.go.tz

# Yaliyomo

04 Ujumbe wa Mkurugenzi Mkuu




05 Tanzania yajiimarisha kama kitovu cha Posta Afrika




Makala kuu

10 TEHAMA kuibadili posta Afrika



12 Kuendeleza biashara mtandaoni Tanzania




13 Kuwa Salama Mtandaoni



Vidokezi kwa watumiaji

17 Jengo la PAPU laakisi mabadiliko ya kidijitali Afrika



BARUA YA MHARIRI

# Karibu Mpendwa Msomaji, Pata nakala za bure ya Regulator kujielimisha

Karibu sana mpendwa Msomaji.

Jarida hili la Regulator ni mojawapo ya nyenzo zinazotumiwa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kuongezaa kiwango cha elimu ya umma na uelewa wa masuala ya sekta zinazosimamiwa, zikiwemo mawasiliano ya simu, huduma za posta na utangazaji.

Jarida pia linawezesha kueneza taarifa muhimu kuhusu majukumu ya Mamlaka.

Jarida hili la kila robo mwaka limesanifiwa upya, kuwezesha wasomaji kupata maudhui kwa urahisi na lina michoro, picha, makala fupi na uchambuzi. Regulator sio tu chapisho: ni jukwaa linalowezesha uwasilishaji wa maudhui yanayoingia kwa undani kwenye ulimwengu wa mawasiliano.

Jarida hili lina maudhui yaliyotafitiwa vizuri na kwa undani kwa madhumuni ya kuwawezesha wasomaji kupata habari za masuala yanayojitokeza kwenye sekta ya mawasiliano ya kielektroniki na posta.

Linafafanua masuala haya,yakiwemo tekinolojia mpya na mabadiliko kwenye sera na mifumo ya usimamizi pamoja na namna hali ya soko la mawasiiano inavyobadili sekta. Lina mwelekeo mpya, uchambuzi wa ndani na maudhui yanayofikirisha kwa namna yanavyohabarisha, kushirikisha na kutia moyo.

Jarida liko mbele kwenye kujenga mwelekeo wa majadiliano na kukuchangia katika kuwezesha maamuzi kwenye sekta ya mawasiliano. Kwa

kusoma Regulator, utaungana na jamii ya watu wenye fikra na maoni kama yako ambao wana hamasa ya kuhakikisha maendeleo ya sekta ya mawasiliano.

Maudhui ya jarida yanakuwezesha kupitia na kupata stadi mpya na pia kupanua mtandao wako wa watu wenye weledi kama wewe. Maudhui ya jarida hili yanaendeleza mjadala na yanashirikisha wahusika wengi zaidi kwenye sekta ya mawasiliano.

Ili kuwezesha mjadala wa masuala yanayojitokeza, tunakaribisha maoni na hoja kutoka kwa wasomaji wetu. Kupata nakala za bure za jarida hili na kuwasilisha maoni, tuma barua pepe kwa: barua@tcra.go.tz.

Kwa maelezo zaidi tafadhali piga simu ya bure kwenye namba ya wateja wa TCRA, ambayo ni 0800008272.



UJUMBE WA MKURUGENZI MKUU

# Kurasa mpya kimawasiliano



Dkt. Jabiri K. Bakari, Mkurugenzi Mkuu wa TCRA

Robo mwaka ya Julai hadi Septemba 2023 imesheheni matukio makubwa katika sekta ya mawasiliano.

Matukio hayo nipamoja na ujio wa mkongo wa nne wa kimataifa wa mawasiliano ya kasi, uzinduzi wa jengo jipya la Umoja wa Posta Afrika (PAPU), kuboreshwa sera ya taifa ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) na mikakati ya kuendeleza biashara mtandao vimeweka alama nyingine za kudumu katika sekta ya mawasiliano Tanzania.

Mkongo huo wa nne, unaoitwa 2Afrika unaungana na ile iliyotangulia; yaani EASSy, SEACOM na SEAS kuingia Tanzania na hivyo kuunganisha na mkongo wa taifa wa mawasiliano ya kasi ambao huduma zake si tu zinatumika nchini bali pia zinatumiwa na nchi jirani zinazotuzunguka.

Jengo la PAPU, makao makuu ya Umoja huo jijini Arusha, ni mradi wa ubia wa mfano kati ya Umoja huo na Serikali ya Tanzania, kupitia TCRA.

Kipindi hiki pia kimeshuhudia kutolewa Kanuni za kusimamia huduma za utangazaji za jamii, yaani huduma zinazotolewa bila kipato kwa watu wanaoishi eneo moja la kijiografia na wenye sifa za kipekee au maslahi ya pamoja.

Kanuni hizi zinatoa miongozo kwa waombaji leseni za huduma za utangazaji za jamii. Zinaainisha umiliki na uendeshaji vituo vya huduma za utangazaji wa jamii, maudhui yanayopaswa kutolewa na vituo hivi, na masuala ya kiufundi. Vyote hivi vimekuja wakati Tanzania ikitekeleza mpango kabambe wa kuibadili kuwa ya kidijitali kwenye maeneo mengi, na kuendeleza utoaji maudhui ya utangazaji kwa Matukio hayo yote kuzingatia weledi, maadili na kanuni husika.

Vilevile TCRA imeendelea kuweka mazingira bora ya kuvutia uvumbuzi wa kidijiti nchini kwa kutoa rasilimali za mawasiliano bila malipo kwa kampuni zinazochipukia katika sekta ya teknolojia ya habari na mawasiliano.

Rasilimali hizo ni pamoja na namba pamoja na masafa ya mawasiliano. TCRA inawahimiza wajasiriamali vijana, wabunifu, na watafiti kuwasilisha mawazo yao ya kibunifu Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania (COSTECH), ili kwanza kupata idhini ya taasisi hiyo kwa shughuli wanayokusudia kufanya, kabla ya kuomba raslimali hizo TCRA.

> **TCRA imeendelea kuweka mazingira bora ya kuvutia uvumbuzi wa kidijiti nchini kwa kutoa rasilimali za mawasiliano bila malipo kwa kampuni zinazochipukia katika sekta ya teknolojia ya habari na mawasiliano.**

Rasilimali za mawasiliano ni msingi wa upatikanaji wa huduma za kielektroniki na posta.

Upangaji na ugawaji wake unawezesha huduma za mtandao zenye kasi kubwa, jambo muhimu katika uchumi wa kidijitali.

MAKALA KUU

# Tanzania yajiimarisha kama kitovu cha Posta Afrika

Na Mwandishi wetu

Tanzania imejiimarisha kama kitovu cha mawasiliano kwa posta Afrika kufuatia kufunguliwa kituo cha kimataifa cha teknolojia ya sekta hiyo na ofisi ya kanda ya Umoja wa Posta Uimwenguni (UPU) jijini Arusha.

Hayo yote yameambatana na kukamilika jengo la kisasa la Umoja wa Posta Afrika (PAPU), ambalo lilifunguliwa na Rais, Dkt Samia Suluhu Hassan Septemba 2023 kwenye jiji hilo ambalo linajulikana kama Geneva ya Afrika.

Tanzania imeweka miundombinu muhimu ya huduma za posta zinazowezeshwa na ubunifu, ikiwa ni pamoja na mfumo wa anwani za makazi na postikodi ambao unatarajiwa kuwezesha ufikishaji na uchukuaji vitu vinavyonunuliwa mitandaoni na kuhitajika kufikishwa kwenye makazi au ofisi za wahusika.

Taasisi nyingi za posta ulimwenguni, likiwemo Shirika la Posta Tanzania (TPC), zinajihusisha na huduma ya vitu vinavyonunuliwa kupitia biashara mtandao.

Nchi za Afrika zinaendeleza biashara inayovuka mipaka yao kupitia mitandao ya posta ya nchi wanachama wa PAPU. Maendeleo ya hivi karibuni kwenye sekta ya mawasiliano yanaonesha kuwa Tanzania, ambayo imezungukwa na nchi nane kati ya hizo tano zikiwa hazina mwambao wa bahari iko kwenye nafasi ya kimkakati ya kufaidi matunda ya biashara mtandao moja kwa mona na kupitia shughuli kwenye hatua mbalimbali za utoaji huduma za posta.

UPU inahimiza na kuendeleza ushirikiano wenye tija ya wadau kwenye mlolongo wa shughuli za posta na ina mkakati wa kutoa motisha kwa watoa huduma za posta na wasimamizi kushirikisha wadau wengine.




*Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan akimkabidhi Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dkt. Jabiri Kuwe Bakari hati ya kutambua mchango wa Mamlaka kwa Hazina. Hafla hiyo ilifanyika wakati wa mkutano ulioandaliwa na Msajili wa Hazina jijini Arusha.*

Miongoni mwa wadau hao ni mashirika ya ndege, wakala wa meli, wasafirishaji, kampuni za ugavi na usafirishaji, mamlaka za usalama na forodha.

Wadau kwenye mlolongo wa huduma za posta wanawezesha shughuli za usafirishaji wa vitu kuwa na ufanisi na kufanyika kwa usalama na hivyo kuwezesha biashara za kimataifa.

UPU imeweka vigezo, kanuni, michakato, viwango na zana za kidijitali kuwezesha ubadilishanaji wa taarifa miongoni mwa wahusika kwenye usafirishaji wa vitu kwa posta.

Tanzania inaimarisha shughuli za usafirishaji mizigo kwa ndege na shirika lake la ndege Air Tanzania lina ndege kubwa ya mizigo iliyoingia nchini hivi karibuni. Inasafirisha mizigo ndani ya Afrika na sehemu nyingine ulimwenguni; hivyo kuiweka Tanzania kwenye nafasi kubwa ya kunufaika na utaratibu huu.

UPU itafungua ofisi yake ya kanda ya Afrika Mashariki kwenye jengo la PAPU jijini Arusha na pia itawezesha kituo cha kujenga uwezo wa wadau kwenye matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA).

Bwana Masahiko Metoki, Mkurugenzi Mkuu wa UPU alisema kwenye sherehe za ufunguzi wa jingo hilo kwamba kituo hicho kitahudumia nchi 45 wanachama wa PAPU.

Katibu Mkuu wa PAPU, Bwana Sifundo Chief Moyo alisema kituo hicho kinatarajiwa kuendeleza ujuzi na stadi za kuendesha shughuli za posta, ikiwa ni mapja na kuhudumia wateja na kuendeleza masoko katika kipindi cha mabadiliko makubwa ya teknolojia.

Tanzania, ambayo ni mwanachama wa Baraza la Utendaji la UPU na PAPU mtawalia, inatekeleza mipango iliyoanzishwa na taasisi hizi kubadili huduma za posta Afrika ziwe chachu ya maendeleo shirikishi ya kiuchumi baraniBarani.

TPC imeanzisha katika posta kadhaa Tanzania vituo vya huduma za kiserikali na umma kwa wananchi. Mpango huo ni sehemu ya kutekeleza mradi wa Tanzania ya kidijitali ambao unalenga kujenga mwelekeo tawala wa TEHAMA kwenye utoaji huduma za serikali.

TCRA inashirikisha wadau wa Sekta ya Posta kuhimiza utekelezaji wa mwelekeo wa UPU wa kufungua UPU kwa wadau wengine.

Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dkt Jabiri Kuwe Bakari ameeleza kuwa kufunguliwa kwa UPU kunafuatia mageuzi ya sekta ya posta, ambayo yamesababishwa na kuwepo kiwango kikubwa cha mwingiliano wa huduma za posta na huduma nyingine, ubinafsishaji wa mashirika ya posta na kuongezeka kwa shughuli za biashara ya mtandao duniani.



*Maafisa waandamizi wa Taasisi ya Mawasiliano ya Kitaifa ya Msumbiji (INCM) walipotembelea TCRA hivi karibuni kujifunza zaidi masuala ya usimamizi. Maeneo waliyopitishwa ni pamoja na utoaji leseni, usimamizi wa huduma za mtandao, upangaji na ugawaji wa rasilimali kama vile namba na masafa. Mengine ni usimamizi wa Usalama mtandaoni, utoaji wa leseni za mawasiliano, usimamizi wa mawasiliano ya simu na Intaneti, huduma za Utangazaji na posta.*

# Mkongo wa nne waingia Tanzania

Na Mwandishi wetu

Mkongo wa kimataifa wa faiba unaopita baharini umeingia Tanzania kipindi ambacho nchi inajizatiti kidijitali.

Agosti mwaka huu, Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan aliongoza sherehe za kufika Tanzania mkongo wa 2Africa, ambao utaunganishwa na mkongo wa taifa wa mawasiliano ya kasi (NICTBB).

Sera ya TEHAMA ya 2016, ambayo mchakato wa kuihuisha ulianza 2023, inasisitiza azma ya serikali kuunganisha mikongo ya kimataifa inayoingia nchini kupitia Dar es Salaam na mkongo wa taifa ili kuongeza uwezo wa intaneti ya kasi kimataifa.

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhe. Nape M. Nnauye alisema Bungeni Mei 2023 kuwa Serikali imetenga fedha kuweka kilometa 60 za waya kupiia Ziwa Tanganyika ili kuiunganisha Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo kwenye NICTBB.

Mkongo wa taifa umefika kwenye mipaka yote ya Tanzania na majirani.




*Ramani ya mkongo wa taifa ya mawasiliano ya kasi (NICTBB)*

Kuna vituo kwenye mipaka ya Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Malawi, Msumbiji na Zambia. Tanzania, kupitia Shirika la Mawasiliano Tanzania, imeingia mkataba na Malawi kuiunganisha na mkongo wa taifa. (Rejea Habari ukurasa wa 16).

Mhe.Nnauye ameeleza ujio wa mkongo wa 2Africa kuwa ni kichocheo kikubwa cha utekelezaji wa mikakati ya kuifanya Tanzania kuwa ya kidijitali. Utaongeza uwezo wa data wa nchi kukidhi mahitaji yanayokua kwa kasi, aliongeza.

Alieleza kwamba pamoja na kuchochea ufanisi katika sekta nyingine nchini na kuongeza mapato ya serikali, mkongo huo utaifanya Tanzania kuwa kitovu cha mawasiliano ukanda wa Afrika; ambalo ni lengo la Sera ya Taifa ya TEHAMA.

Mikongo wa faiba inayopita baharini ina faida zaidi ya mawasiliano ya satelaiti kwa kuwa imetengenezwa kuhakikisha wingi na kasi ya data. Vilevile ina uimara na usalama zaidi n ani vigumu kuidukua.

Haipotezi mawasiliano, ina muingiliano kidogo ya umeme-sumaku na pia haichafui mazingira.

Satelaiti zinaweza kuathiriwa na hali ya hewa.

Hata hivyo mikongo ya baharini haifai kwenye maeneo yenye historia za maafa ya bahari ni kama vile vimbunga vinavyosababisha mawimbi makubwa na tsunami.

Ujenzi wa mikongo unachukua muda mrefu zaidi kuliko satelaiti na ni ghali pia. Vilevile mikongo hii inaweza kuhujumiwa.

# USHIRIKIANO MPYA TCRA, COSTECH

Na Mwandishi wetu

Dar es Salaam, Julai 20, 2023 Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) pamoja na Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania (COSTECH) zimefikia makubaliano kwa lengo la kutoa rasilimali za mawasiliano bila malipo kwa kampuni zinazochipukia katika sekta ya teknolojia za kidijiti. Hatua hii inalenga kuweka mazingira bora ya kuvutia uvumbuzi wa kidijiti nchini na kuhakikisha kuwa kampuni hizo zina nafasi ya kukua na kufanikiwa.

Akizungumza hivi karibuni jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dkt. Jabiri Bakari, alisisitiza kuwa mpango huu unalenga kuwapa vijana wabunifu zana wanazohitaji kwa majaribio ya huduma zao kwa kipindi maalum. "Hapo awali, ili uweze kujaribu kitu chochote katika anga la mtandao, ilibidi upate leseni na kutoa gharama kubwa.

Sasa tunasema kama wewe ni mwanafunzi au mbunifu umeingia kwenye ulimwengu wa kidijiti, umegundua kitu, na umetengeneza kitu kinachoweza kuleta manufaa makubwa, na unataka kukijaribu, na katika kukijaribu unahitaji rasilimali kama namba, masafa, au hata kushirikiana na kampuni za simu; tunasema majaribio kama hayo ni bure," alisisitiza Dkt. Bakari.

Hadi kufikia Juni 2023, TCRA ilikuwa tayari imetoa rasilimali hizi muhimu kwa kampuni nne.

Dkt. Bakari aliwahimiza wajasiriamali vijana, wabunifu, na watafiti kuwasilisha mawazo yao ya kibunifu kwa COSTECH na kuwahakikishia kwamba baada ya idhini kutoka COSTECH, watapata rasilimali hizi bila gharama yoyote.



*Watumiaji wa huduma za mitandao wakiwa kwenye chumba cha kompyuta kwenye mojawapo ya vyuo vikuu Tanzania*

> *kama wewe ni mwanafunzi au mbunifu umeingia kwenye ulimwengu wa kidijiti, umegundua kitu, na umetengeneza kitu kinachoweza kuleta manufaa makubwa, na unataka kukijaribu, na katika kukijaribu unahitaji rasilimali kama namba, masafa, au hata kushirikiana na kampuni za simu; tunasema majaribio kama hayo ni bure*
>
> — Dkt. Jabiri K. Bakari

Rasilimali za mawasiliano ni msingi wa upatikanaji wa huduma za mawasiliano, kama vile huduma za pesa za simu na huduma nyingine zinazotegemea teknolojia za kidijitali kama vile kilimo cha kisasa, biashara mtandao, usafirishaji, uendeshaji wa taasisi binafsi miongoni mwa zingine.

"Ugawaji wa rasilimali hizi unawezesha huduma za mtandao zenye kasi kubwa, jambo muhimu katika uchumi wa kidigitali," alisisitiza Dkt. Bakari na kuongeza kuwa wabunifu wenye bunifu zinazoleta Suluhu kwa changamoto za jamii sasa wataweza kushirikiana na TCRA, COSTECH na Watoa huduma hasa mitandao ya simu ili kuzibeba bunifu hizo.

Miongoni mwa rasilimali zinazotolewa na TCRA ni pamoja na rasilimalinamba (numbering resources), masafa (frequency spectrum), postikodi, na anwani za makazi.

Mkurugenzi Mkuu wa TCRA alisema mpango huu ni endelevu na kuwa TCRA na COSTECH wanahimiza wajasiriamali vijana, wabunifu, na watafiti kuwasilisha mawazo yao ya kibunifu kwa COSTECH.

Baada ya kupata idhini, watapata rasilimali hizi bila gharama yoyote na kuzitumia kwa kipindi cha majaribio ya miezi mitatu pamoja na uwezekano wa kuongezewa muda wa kufanya majaribio yao.

Meneja wa Chama cha Wabunifu, Tanzania Start-Ups Association (TSA), Praygod Japhet, akizungumzia mpango huu alisema kuwa, hapo awali rasilimali hizo za mawasiliano zililipishwa kwa kiwango kikubwa, mara nyingi hadi kufikia milioni kumi kulingana na huduma.

Lakini sasa, kwa ushirikiano wa TCRA na COSTECH, wabunifu chipukizi wanapata rasilimali hizo bila malipo.

"Hii imesaidia kupunguza mzigo kwa wabunifu wengi, ambao mara nyingi ni vijana kutoka vyuo vya kati na vikuu, na ambao wamekabiliana na changamoto za upatikanaji wa mitaji. Hatua hii inaleta rasilimali adimu na za gharama kwa wabunifu, ambazo zitasaidia kuboresha jamii ya Watanzania," alisisitiza.

Mkuu wa Kitengo cha Habari wa COSTECH, Mary Kigosi, alisema kuwa ushirikiano kati ya taasisi yao na TCRA umesaidia sana kupunguza changamoto kwa wabunifu wa teknolojia ya kidijiti ambao hapo awali walikuwa wanakabiliana na changamoto ya kupata zana hizi muhimu kwa maendeleo yao.

"Rasilimali za namba na masafa, kwa mfano, ni muhimu sana kwa wabunifu wa teknolojia ya kidijiti katika sekta za kilimo, ujasiriamali, biashara mtandao, suluhu za kielimu, na zaidi.

Hata hivyo, wabunifu walikuwa wanakabiliwa na changamoto ya kuzipata hapo awali, lakini baada ya makubaliano kati yetu na TCRA, sasa wanapata rasilimali hizi bila malipo, na hii ni hatua kubwa kwa Tanzania katika enzi hizi za ulimwengu wa kidijitali," alifafanua.

> *Hii imesaidia kupunguza mzigo kwa wabunifu wengi, ambao mara nyingi ni vijana kutoka vyuo vya kati na vikuu, na ambao wamekabiliana na changamoto za upatikanaji wa mitaji.*
>
> *— Praygod Japhet*
>
> *Meneja wa Chama cha Wabunifu, Tanzania Start-Ups Association (TSA)*

# TEHAMA kuibadili Posta Afrika




*Wajumbe kutoka nchi mbakllimbali za Afrika walioshiriki mkutano wa Baraza la Utawala la Umoja wa Posta Afrika (PAPU) jijini Arusha tarete 30 Agosti, 2023.*

Mkutano huo ulitanguliwa na sherehe ya uzinduzi wa jengo la PAPU uliofanywa na Dkt. Rais Samia Suluhu Hassan tarehe 2 Septemba.

> ***Posta za Afrika zinatekeleza Mkakati wa Posta wa Abidjan, uliopitishwa na Umoja wa Posta Ulimwenguni (UPU) Agosti 2021.***

Mkakati huo wa mwaka 2022 hadi 2025 unatambua umuhimu wa sekta ya posta katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi, ambapo huduma za posta za sasa zitakuwa na mchango mkubwa kuliko miaka ya nyuma.

Vilevile unaeleza kwamba Posta za Afrika zina nafasi nzuri zaidi kutumia mitandao kutoa huduma za kiutawala kiutawala, biashara na fedha kwa makundi ambayo wanaweza kusahaulika kiurahisi kama vile wanawake, watu masikini, wasio na elimu ya kutosha na walio kwenye sekta isiyo rasmi.

Mkakati wa Posta wa Abidjan unalenga kuchochea maendeleo na upatikanaji wa huduma za posta zenye ufanisi ili kuhakikisha kwamba vitu vinavyosafirishwa kwa posta vinafikishwa kwa urahisi kupitia mfumo wa posta uliounganika kwenye eneo moja na unaotumia mitandao iliyounganishwa.

Malengo yake mengine ni kuhamasisha matumizi ya viwango vinavyokubaliwa na watu wengi, pamoja na teknolojia; kuhakikisha kwamba kunakuwa na ushirikiano na muingiliano miongoni mwa wadau na kuendeleza ushirikiano wa kiufundi wenye tija.

Lengo ni kuhakikisha kwamba huduma za Posta zinakidhi mahitaji ya wateja ambayo yanabadilika.

Alifunga mkutano huo, Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohammed amezitaka Posta za Afrika kutumia fursa zinazotokana na kukua kwa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika huduma zao.

# Huduma za posta na usafirishaji wa vipeto




**651,928**

Vitu vilivyosafirishwa kupitia Shirika la Posta Tanzania (TPC)

**152,584**

Vitu vilivyotumwa kupitia wasafirishaji vifurushi (courier)

Vitu vingi zaidi vilisafirishwa kwenye maeneo ya ndani, ikifuatiwa na Afrika Mashariki na duniani kote (Row)

Vitu vingi vilisafirishwa kwenye maeneo ya ndani kuliko kwenye maeneo ya kimataifa. idadi ya vitu vilivyosafirishwa imepungua kadri muda unavyopita

**Vitu vilisafirishwa zaidi duniani kote (RoW) kuliko Afrika Mashariki (EAC )**



**Vitu vingi vilisafirishwa kupitia posta (TPC)**

**9,909**

**Vilivyosafirirshwa kwenda EAC**

**97,238**

**Vilivyosafirishwa kutoka EAC**

Ameongeza kuwa kutokana na kukua kwa TEHAMA bara la Afrika linaweza kubadilishana bidhaa kwa njia ya posta bila vikwazo vya mipaka, hiyo kuendeleza biashara mtandao.

> ***Kutokana na kukua kwa TEHAMA bara la Afrika linaweza kubadilishana bidhaa kwa njia ya posta bila vikwazo vya mipaka, hiyo kuendeleza biashara mtandao.***
>
> **Dkt. Khalid Salum Mohammed**
>
> *Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar*

Amehimiza hatua za kuwajengea uwezo wataalamu wa Posta, kutoa elimu kwa umma na kujenga miundombinu ya kidijitali ili kuunganisha maeneo yote ya mijini na vijijini katika katika nchi husika.

Usalama wa huduma mtandao pia imarishwe, amesisitiza.


# Kuendeleza biashara mtandao Tanzania

Kijiografia, Tanzania ina nafasi kubwa ya kundeleza biashara mtandao Afrika. Ina mwambao ambao umefikiwa na mikongo mingi ya mawasiliano na mkongo wa taifa umefika mipakani.

Faida za kiuchumi za biashara mtandao kwa Tanzania zimeelezwa kwenye ripoti ya hivi karibuni ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Biashara, Uwekezaji na Maendeleo (UNCTAD).

Hizo ni pamoja na kujenga uchumi kwa kuzalisha ajira, kunzisha vyanzo vipya vya mapato na kuwezesha shughuli nyingine zinazoambatana na biashara mtandao.

Ripoti hiyo inahimiza uwepo wa sera na kanuni zinazoongoza biashara mtandao na kuifanya kuwa mwelekeo tawala kwenye shughuli nyingine za uchumi na biashara.



Pamoja na mitandao ya TEHAMA, miundombinu mingine muhimu kwa biashara mtandao ni mfumo wa anwani za makazi na postikodi, ambao umeenea Tanzania nzima.

Vilevile Tanzania kuna barabara nzuri maeneo mengi na usafiri wa ndege kwenda miji mikubwa umeboreshwa.

Kuwasili kwa ndege ya mizigo inayomilikiwa na Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) pia utachangia ufanisi wa usafirishaji bidhaa zinazonunuliwa au kusafirishwa nje ya nchi.

Changamoto za matumizi ya intaneti minongoni mwa watu linafatutiwa ufumbuzi. Sera ya TEHAMA inapendekeza hatua kuongeza matumizi ya simu janja na vifaa vya mkononi vinavyowezesha mawasiliano ya intaneti.

Takwimu za mawasiliano za Juni 2023 zilizotolewa na TCRA zinaonesha simu janja zimeenea miongoni mwa Watanzania kwa asilimia 27.

Taasisi ya GSMA, inayowakilisha maslahi ya watoa huduma za mitandao ya mawasiliano ya simu za mkononi inapendekeza mambo matano kufungua fursa za kuendeleza biashara mtandao Tanzania.

1. Kipaumbele kwenye mkakati na mpango kazi, na pia kuratibu shughuli zote zinazohusiana na biashara mtandao.
2. Kuimarisha sheria na kanuni za kumlinda mtumiaji na kuendeleza utoaji elimu.
3. Kupitia upya shughuli za Shirika la Posta Tanzania ili kuboresha ufanisi wake kwenye usafirisha na kuhifadhi vitu vinavyosafirishwa.
4. Kushirikiana na watoa huduma za biashara ngazi zote kueneza uelewa wa faida za kiuchumi watakazopata kuoitia mifumo ya kidijitali.
5. Kuwezesha uimarishaji wa stadi zinazohitajika kuanzisha na kuendesha biashara mtandao kwa mafanikio.

VIDOKEZI KWA WATUMIAJI

# Kuwa Salama Mtandaoni: Jinsi ya kuepuka viunganishi vya kitapeli

Na Mwandishi wetu

Intaneti ni huduma muhimu katika ulimwengu wa leo na imekuwa chachu ya kuwezesha mambo mbalimbali ikiwemo kupata habari, kufanya biashara, na kuwasiliana kwa haraka.

Hata hivyo, licha ya faida nyingi, ulimwengu wa dijitali pia unaleta hatari kwa kuwa wahalifu nao hutafuta njia mpya za kutapeli watu kupitia mitandao. Hatari mojawapo ni matumizi ya viunganishi vya kitapeli vilivyoundwa maalumu kuwadanganya watu na kuwaongoza kwenye tovuti hatari. Hapa chini ni orodha ya viungo hatari, pamoja na maelezo ya jinsi ya kuviepuka.

## 01 Angalia kwa makini mtumaji na ujumbe

Unapaswa kufahamu kuwa mlinzi wa kwanza dhidi ya viunganishi bandia na hatari ni wewe mwenyewe hivyo unapaswa kuwa macho muda wote. Unapopokea ujumbe au barua pepe fuata mwongozo huu:

- Jihadhari na barua pepe au ujumbe usioombwa, hasa zile zinazoanza na salamu za kawaida kama “Mpendwa Mteja.” Biashara halali kawaida huzibinafsisha ujumbe wao.
- Chukua tahadhari na ujumbe unaojaribu kukushinikiza kubofya kiunganishi mara moja kwa kukutengenezea hisia ya haraka au hofu. Wahalifu mara nyingi hucheza na hisia zako.
- Tafuta makosa ya sarufi na utofautishaji wa lugha katika ujumbe. Hizi ni ishara za chanzo bandia, kwa kuwa biashara halali hulinda viwango vya mawasiliano ya kitaalam.
- Kumbuka kuwa biashara zenye sifa haziombi mara kwa mara taarifa za binafsi kupitia barua pepe au ujumbe. Ikiwa ujumbe unauliza taarifa binafsi, kuwa makini.

## 02 Angalia Kiungo Kabla ya Kubofya:

Kwa vile viunganishi vya kitapeli vinaweza kuonekana salama, ni muhimu kutathmini kwa uangalifu kila kiunganishi, kabla ya kubofya. Ili kuepuka na aina hii ya udanganyifu, unaweza kufanya yafuatayo

- Bofya kiungo kuona marudio halisi kwenye mstari wa pili. Viungo vya kitapeli mara nyingi huwa na anwani ama URL zisizolingana na maelezo ya kiungo.
- Kuwa makini na viunganishi vya tovuti (URL) zilizopunguzwa kwani zinaweza kuficha marudio halisi. Tumia huduma salama ya kupanua URL kuona anwani kamili kabla ya kubofya.
- Hakikisha kuwa anwani maarufu za wavuti hazina makosa madogo ya herufi au marekebisho madogo. Wahalifu wa mtandao mara nyingi hujenga nakala zinazovutia za tovuti maarufu.
- Ikiwa huna uhakika, andika anwani ya wavuti moja kwa moja kwenye kivinjari chako badala ya kubofya kiungo. Hii inahakikisha unafikia tovuti sahihi na salama.

## 03 Tumia hatua na zana za usalama:

Zingatia hatua zifuatazo:

Tumia programu ya kuangamiza virusi mtandaoni maarufu kwa kimombo kama “antivirus na anti-malware” ili kulinda kifaa chako kutoka kwa tishio la uwezekano na unaweza kusasisha (update) mara kwa mara programu hizi ili kubaki salama kutokana na hatari mpya.

Endelea kusasisha mfumo wako wa uendeshaji na programu na maboresho ya usalama ya hivi karibuni. Wahalifu wa mtandao hutumia mapungufu katika programu zilizopitwa na wakati.

Boresha usalama kwa kuwezesha uthibitisho wa hatua mbili kwa akaunti zako mtandaoni (Two factor authentication). Hata kama mtu atapata nenosiri lako, mlaghai hatapata akaunti yako bila hatua ya pili.

Epuka kutumia mitandao ya Wi-Fi ya umma kwa data za siri au shughuli za kifedha. Mitandao ya Wi-Fi ya umma mara nyingi haina usalama wa kutosha na ni lango kuu la wahalifu mtandaoni.

Pamoja na hatua hizi za usalama, endelea kuwa macho unapotumia mtandao.

Kuwa mwangalifu, epuka kubofya kwa pupa, na weka usalama wako kwanza. Kwa kufuata vidokezo hivi, unaweza kujilinda dhidi ya viungo vya udanganyifu na kuimarisha usalama wako mtandaoni.

## Majiji ya kidijitali ajenda mkutano wa ITU Arusha

Wataalamu wa teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) wa nchi mbalimbali, chini ya utaribu wa Shirika la Mawasiliano Ulimwenguni (ITU) wameku tana jijini Arusha hii karibuni kujadili masuala saba yanayohusiana na uendelezaji majiji ya kisasa.

Mkutano huo wa wataalamu wanaounda kundi namba 20 la ITU la wataalamu wanaoshughulikia masuala ya vifaaa vinayojiendesha vyenyewe kupitia intaneti, na majiji ya kisasa, ulisisitiza umuhimu wa kuweka misingi itakayohakikisha uendelevu wa majiji ya kisasa.

Mkutano pia ulijadili matumizi ya TEHAMA katika shughuli za uendeshaji na uzalishaji. Masuala yaliyojadiliwa ni usimamizi wa taarifa, mifumo ya usafiri inayotumia TEHAMA, kilimo ufugaji bora kwa kutumia teknolojia za kisasa.

Tanzania inatekeleza mpango wa kubadili majiji ya Dodoma, Arusha na Mbeya kuwa ya kisasa, hivyo kujiunga na majiji maarufu barani Afrika kama vile Cape Town Afrika Kusini ambayo yana hadhi hiyo.

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhe. Nape M. Nnauye ameliambia Bunge jijini Dodoma Mei 19 mwaka huu kwamba wizara yake itafanya tathmini ya kuyafanya majiji hayo kuwa ya kisasa kidijitali.

Madhumuni ni kutabadili maisha ya wakazi wa majiji hayo, aliongeza.

Majiji ya kisasa kidijitali yanakuwa na mifumo ya kielektroniki inayosimamia huduma za umma na za kiusalama ikiwani pamoja na kuwezesha taa za kuongoza magari kubaini mwelekeo wa foleni, mfumo wa kielektroniki wa kukusanya data za matumizi ya umeme, maji na hudma za taka.

Ili jiji liwe la kisasa kidijitali, linahitaji wakazi wake kuwa na uelewa kwenye matumizi ya huduma za kidijitali. Pia linahitaji miundombinu imara, upatikanaji wa masafa ya mawasiliano ya kasi yanayowezesha intaneti ya uhakika, vyanzo vya nishati vinavyoaminika na miundombinu na mifumo wa usafiri.



# Vidokezo mawasiliano kwa intaneti



Intaneti ni mfumo wa mawasiliano kupitia kompyuta zilizounganishwa ulimwenguni. Kompyuta hizo ni pamoja na vifaa vya mawasiliano vyenye uwezo wa kupata huduma za intaneti. Maudhui yanayopita kwenye intaneti yanaitwa data, yakiwa ni herufi au tarakimu.

Data inavyotengenezwa kwa ajili ya kutumwa inaitwa ujumbe. Kabla ujumbe haujatumwa, unagawanywa vipande vidogo sana vinavyoitwa vifurushi.

Hivi vinasafirishwa kupitia Itifaki ya Intaneti, yaani utaratibu wa intaneti na mfumo wa Udhibiti wa Usafirishaji wa hivyo vifurushi. Itifaki hii inatiwa 'internet protocol', kwa kifupi IP. Ndiyo maana kuna kitu kinaitwa anwani ya IP.

Kwa upande wa anayepokea ujumbe, vifurushi hivyo vilivyofumuliwa vinaunganishwa tena na kuonekana kama ujumbe kamili.

Vifurushi kwenye ujumbe vinatokana na herufi au tarakimu. Kwenye matumizi ya kompyuta, herufi au tarakimu moja vinaitwa baiti.

Neno TCRA lina baiti nne. Zikiwa 100 ni kilobairi (KB), elfu ni megabaiti (MB), milioni ni gigabaiti (GB) na bilioni ni terabaiti (TB).

Kasi ya mtandao inapimwa kwa muda utaotumika kutuka ujumbe. Hivyo kwa kasi ya terabaiti 17 kwa sekunde ya mkongo wa 2Africa maana yake ni herufi bilioni 17 kwa sekunde.

**Kwenye matumizi ya kompyuta, herufi au tarakimu moja vinaitwa baiti**

| | | |
|---|---|---|
| 1 | Baiti | B |
| 100 | Kilobaiti | KB |
| 1,000 | Megabaiti | MB |
| 1,000,000 | Gigabaiti | GB |
| 1,000,000,000 | Terabaiti | TB |

**mkongo wa 2Africa una kasi ya terabaiti 17 kwa sekunde**

# Mkongo wa Tanzania wafika Malawi

Shirika la Mawasiliano Tanzania - TTCL limesaini Mkataba wa Makubaliano ya Kibiashara na Kampuni ya Serikali ya Nchini Malawi inayosimamia Mkongo wa Mawasiliano - Electricity Supply Corporation of Malawi Limited (ESCOM) tarehe 8 Septemba, 2023 Kijangwani Zanzibar.

Mkataba huo umesainiwa na Mkurugenzi wa TTCL, Mhandisi Peter Ulanga pamoja Mtendaji Mkuu wa ESCOM, Bw. Kamkwamba Kumwenda na kushuhudiwa na Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mhe. Nape Nnauye (Mb) , Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Mhe. Khalid S. Mohamed na Waziri anayesimamia Mawasiliano kutoka Serikali ya Malawi (Ministry of Information and Digitalisation) Mhe. Moses Kunkuyu Kalongashawa.

Mkataba huo umetokana na ziara aliyoifanya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan alipofanya mapema mwaka huu Malawi.

Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano unakusudiwa kuongeza wigo wa mawasiliano ya simu na intaneti Tanzania na nchi jirani katika kuharakisha mapinduzi ya kidijitali.

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhe. Nape N. Nnauye (Mb) alisema Bungeni mwezi Mei mwaka 2023 kwamba Serikali imetenga fedha kuweka kilometa 60 za waya kupitia Ziwa Tanganyika ili kuiunganisha Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo kwenye mkongo wa taifa wa mawasiliano.

Vilevile Serikali itakamilisha ujenzi wa kilomita 1,600 za Mkongo na vituo vipya 15 vya kutolea huduma za na vituo vipya vitajengwa ili kuongeza wigo wa utoaji wa huduma ngazi za wilaya Tanzania.




*Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL), Mhandisi Peter Ulanga (kushoto) akiweka saini kwa niaba ya Tanzania makubalkiano ya kufikisha Malawi mkongo wa taifa wa mawasiliano ya kasi.*

# Jengo la PAPU laakisi mabadiliko ya kidijitali Afrika

Mfano wa mchango kwenye juhudi za sekta ya Posta Afrika kuelekea mabadiliko kidijitali kwenye utoaji huduma unaonekana Arusha, kupitia jengo la kisasa litakalokuwa makao makuu ya taasisi mahsusi kwa kushughulikia masuala ya posta katika Bara hili.


Umoja wa Posta Afrika (PAPU), ambao unatekeleza mikakati ya kuendeleza biashara mtandaao Barani humu, sasa umepata jengo la makao makuu lililojengwa kwa mabilioni ya shilingi na ambalo ni kivutio kwa usanifu na mwonekano wake, ulio kama stempu.

Jengo hilo jipya, lenye nafasi ya ofisi na maeneo ya biashara, na ambalo linaendeshwa kwa teknolojia za kisasa, litazinduliwa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan tarehe 2 Septemba mwaka huu. Kwa Arusha, jiji linalojulikana kwa sifa ya kuwa kituo cha mikutano ya kimataifa kama vile ilivyo Geneva, jengo hilo ni johari nyingine kwenye taji lake.

Tanzania iijitolea kuwa mwenyeji wa PAPU Umoja huo ulipoanzishwa tarehe 18 Januari 1980 mjini Arusha. Jengo hili jipya la PAPU limejengwa kwa ubia kati ya Umoja huo na Serikali ya Tanzania kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania.

Umiliki ni asilimia 60 PAPU na 40 TCRA. TCRA, msimamizi wa sekta ndogo ya posta nchini, ni mdau mkuu katika mradi huu na inawakilisha Serikali kwenye masuala ya kuhudumia PAPU.

**Umiliki wa jengo la PAPU**






*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akimkabidhi Katibu Mkuu wa Umoja wa Posta Afrika (PAPU) Dkt. Sifundo Chief Moyo mfano wa ufunguo wa jengo la Umoja huo lililojengwa jijini Arusha kwa ushirikiano na Serikali ya Tanzania, baada ya kulifungua rasmi Septemba 2023.*

Kukamilika kwa jengo hili kumewezekana miaka mitatu baada ya kuwekwa jiwe lake la msingi, sherehe iliyofanyika tarehe 18 Janauari 2020, wakati wa maadhimisho ya miaka 40 ya PAPU.

Aliyekuwa Waziri wa Tanzania wa Ujenzi, Usafirihaji na Mawasiliano, Mhandisi Isack Kamwelwe, aliweka jiwe hilo kwa niaba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Jengo hili limebadilisha mandhari ya jiji la Arusha. Mfano wa stempu ya kidijitali unaonekana kwa wanaoingia jiji hili kutoka sehemu tofauti na ukiwa juu yake unapumua hewa safi na kuona jiji la Arusha kwa chini, ikiwa ni pamoja na ardhi na mashamba,miti na bustani na vijito vinavyotiririka maji kutoka Mlima Meru, ambao ni wa pili kwa urefu Tanzania baada ya Kilimanjaro ulio jirani.

Majengo ya PAPU yako katika mita za mraba 22,421; kando ya barabara kuu kutoka Moshi kuelekea Namanga kwenye mpaka wa Tanzania na Kenya. Arusha ni lango kuu cha kuingilia maeneo ya vivutio vya kitalii, vikiwa ni pamoja na mbuga ya wanyamapoti ya Serengeti na eneo la uhifadhi la Ngorogoro, ambalo litambuliwa kimataifa kama Urithi wa Dunia.

Huduma nyingi kwenye jengo hilo la PAPU zinaendeshwa kwa kutumia tenolojia ya kisasa, ambazo zinawezesha mtumiaji kupata huduma kwa ufanisi wa hali ya juu.

Jengo kuu lenye ghorofa 17 lina sehemu ya chini ya ardhi, ofisi za kisasa, eneo la shughuli za biashara na maegesho yenye uweo wa magari 137, yaani 37 hilo eneo la chini ya ardhi na 130 kuzunguka jengo. Kuna seti tatu za majenereta ya umeme kwa ajili ya dharura. Pia kuna matenki ya kufadhia maji ya juu ya paa yenye uwezo wa ujazo wa lita 7,200 na chini ya ardhi yenye uwezo wa lita 210,000.

Vilevile kuna ukumbi wa mikutano wenye vifaa vya kisasa vya kidijitali, unaoweza kuingia washiriki 400 kwa mara moja. Pia kuna vyumba vitano vya mikutano midogo vyenye uwezo wa washiriki 30 kila kimoja.

Uamuzi wa kuwa na jengo la kisasa la PAPU ulifanyika kwenye mkutano wa 29 wa kawaida wa mawaziri wa uliokuwa Umoja wa Nchi Huru Afrika (OAU), ambao sasa ni Umoja wa Afrika (AU) Julai 1977 jijini Libreville, Gabon. Walipitisha azimio namba CM/Res. 586(XXIX) ambalo lilipendekeza kuanzishwa kwa PAPU kuwa chombo cha juu cha kusimamia masuala ya Posta Afrika.

Azimio hilo liliidhinishwa na Wakuu wa Nchi na Serikali wa OAU kwenye mkutano wao mkuu uliofanyika Libreville Julai 1977.



Tarehe 7 Oktoba 1984, PAPU na Serikali ya Muungano wa Tanzania ziliingia mkataba ulioainisha masharti na vipengele vingine vya kuweka makao makuu ya Moja huo Arusha. Hili lilifuatia kutolewa idhini na aliyekuwa Rais wa Tanzania, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere tarehe 24 Septemba 1984; hivyo kufungua njia ya PAPU kuwa na makao yake makuu Arusha.Kwa kipindi kirefu, huduma za Posta Afrika zimekuwa na majukumu ya kipekee, kabla ya ukoloni, wakati wa ukoloni na baada ya nchi za bara hili kujipatia uhuru.

Katika ujumbe wake siku ya Posta Afrika tarehe 18 Januari 2023, Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dkt. Jabiri K. Bakari alieleza kwamba ushirikiano baina ya nchi kupitia huduma za Posta umekuwa na umuhimu mkubwa katika kujenga mazingira ya biashara. Ili kufanikisha na kuwezesha hili, Tanzania hivi karibuni imekaribisha uwezeshaji wa huduma za posta kati yake na nchi nyingine kupitia mipaka.

PAPU inasisitiza utayari wake wa kubadili huduma za Posta Afrika kuwa kichocheo cha biashara mtandao kati na baina ya nchi.

Katibu Mkuu wa Umoja huo, Bwana Sifundo Chief Moyo alisema kwenye ujumbe wake Siku ya Posta Afrika mwaka huu kwamba hili litawezekana kupitia mabadiliko ya kidijitali katika uendeshaji shughuli za posta na kuzifanya kuwa za kisasa kwa kutumia teknolojia ili kufungamanisha utoaji wa huduma.

Posta imechukua mwelekeo tofauti kufuatia kushuka kwa idadi ya barua na kuongezeka kwa vifurushi vinavyosafirishwa kama sehemu ya biashara mtandao. Sekta ya Posta inabidi kuelekeza juhudi zake, kupanga upya uwezo na mwelekeo wake na pia raslimali zake, ili kujiweka tayari kutoa huduma kama chombo kinachotegemewa kusafirisha vitu na kufikisha huduma, alifafanua.

Posta zinatakiwa kuchukua fursa ya kukua kwa biashara mtandao na masoko yanayojitokeza kuongeza vyanzo vya mapato yao na kujijengea uhalali miongoni mwa jamii zinapotoa huduma. Vituo vya posta zaidi ya 37,000 vilivyoenea Barani Afrika ni sehemu za kuanzia kupanua huduma kuoitia mifumo ya kidijitali kuelekea kuwa na posta zenye hadi za kisasa, alisema Katibu Mkuu huyo.


“Kwa kupata na kutumia programu za kidijitali kuendesha posta na kutoa huduma kupitia intaneti na vifaa vya mkononi kama vile simu janja, vishkwambi, komputa mpakato, Posta zinaweza kuongeza uwezo wa kutoa huduma kwa uganisi zaidi.” aliongeza.




*Rais akimpongeza Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dkt.Jabiri K. Bakari (kushoto) kwa usimamizi mahiri wa ujenzi wa jengo la PAPU wakati Rais alipotembelea ofisi za Mamlaka ndani ya jengo hilo siku ya uzinduzi. Katikati ni Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhe. Nape M. Nnauye.*

# Sekta ya Mawasiliano katika namba

## Umiliki wa soko kwa watoa huduma




## Kiwango cha ongezeko la wateja wa mawasiliano (kwa robo mwaka)




## Idadi ya watumiaji wa simu

| Mtoa huduma | Juni | Julai | Agosti | Septemba |
|---|---|---|---|---|
| Airtel | 17,505,139 | 17,924,973 | 18,426,704 | 18,485,232 |
| Tigo | 17,484,387 | 17,505,562 | 17,756,672 | 18,181,259 |
| TTCL | 1,559,090 | 1,585,879 | 1,606,925 | 1,621,049 |
| Smile | 13,840 | 13,724 | 13,404 | 7,826 |
| Halotel | 8,410,029 | 8,332,702 | 8,436,839 | 8,266,320 |
| Vodacom | 19,116,166 | 19,732,390 | 20,165,204 | 20,555,763 |
| **Jumla** | **64,088,651** | **65,095,230** | **66,405,748** | **67,117,449** |



**35%**


Hakuna mtoa huduma anayemiliki zaidi ya 35% ya soko, ambayo ni kiwango cha chini zaidi kwa mtoa huduma mkuu



**Ushindani wenye tija**

Uchunguzi unaonyesha hakuna mtoa huduma anayetawala, inaashiria uwepo wa ushindani wenye tija baina ya watoa huduma

### Mabadiliko ya watumiaji kulingana na mtoa huduma




### Hatua za kistoria

**9%** — Mwenendo wa usajili wa huduma za mawasiliano kwa miaka mitano iliyopita unaonesha ongezeko la wastani kwa 9% kila mwaka

**109%** — Hadi kufikia Septemba 2022 ueneaji wa huduma umefikia 109% kiwango cha juu kabisa katika historia